

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA KUMI NA NANE

09 MEI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA KUMI NA NANE – TAREHE 09 MEI, 2022

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

150. MHESHIMIWA CHARLES MUGUTA KAJEGE (MWIBARA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itanza kukarabati Shule za Msingi za Nansimo, Kenkombyo, Kitengule na Namibu katika Jimbo la Mwibara.

**151. MHESHIMIWA OMARI MOHAMED KIGUA
(KILINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itapeleka Gari la Wagonjwa katika Wilaya ya Kilindi.

**152. MHESHIMIWA ENG. EZRA JOHN CHIWELESA
(BIHARAMULO MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itarejesha Shilingi Milioni 204 iliyorudishwa Mwaka 20019/2020 ili kukamilisha ujenzi wa Hospitali Biharamulo.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA
MAZINGIRA)**

**153. MHESHIMIWA JESCA JONATHAN
MSAMBATAVANGU (IRINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali ina Mpango gani wa kurudisha uoto wa asili wa milima ya Iringa ili kuendelea kutunza mazingira yake na vyanzo vya maji.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

154. MHESHIMIWA BONIVENTURA DESTERY KISWAGA (MAGU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha VETA katika Wilaya ya Magu.

WIZARA YA AFYA:

155. MHESHIMIWA ZAYTUNI SEIF SWAI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani kuboresha huduma za afya kwa Wazee wa Mkoa wa Arusha kwa kuwapatia dawa kupitia mfumo wa bima.

156. MHESHIMIWA KHALIFA MOHAMED ISSA (MTAMBWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupambana na Magonjwa yasiyoambukiza.

WIZARA YA NISHATI:

157. MHESHIMIWA BERNADETA KASABAGO MUSHASHU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni Vijiji vingapi havijapatiwa umeme wa REA na nini mpango wa Serikali kusambaza umeme kwenye Vijiji vyote vya Mkoa wa Kagera.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:-

158. MHESHIMIWA ALI HASSAN OMAR KING (JANG'OMBE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, TRA itasitisha lini kukusanya na kuzirudisha fedha za VAT ilizokusanya kutoka kwenye miamala ya mtandaoni iliyofanywa Zanzibar.

**WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA
BIASHARA:**

**159. MHESHIMIWA JUDITH SALVIO KAPINGA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji,
Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali kupitia Tume ya Ushindani (FCC) ina
mkakati gani wa kumlinda Mlaji katika biashara
za mtandaoni.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

**160. MHESHIMIWA INNOCENT SEBBA
BILAKWATE (KYERWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na
Uchukuzi:-

Je, ni lini ujenzi wa kilomita 50 za barabara ya
Mugakorongo kuanzia mpaka wa Uganda na
Tanzania utaanza ili kuvutia biashara na Watalii.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

(Majadiliano yanaendelea)

09 MEI, 2022
DODOMA

N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE